
# ELIMIKA NA ZBS

## UKAGUZI WA BIDHAA NA MUELEKEO WA UINGIAJI WA BIDHAA BORA

Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) ni chombo kilichowekwa kisheria ili kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi na zile zinazoingizwa nchini zinakuwa katika viwango venye kukidhi ubora uliokusudiwa na kubaki salama kwa ajili ya matumizi ya wananchi na mazingira yao.

Katika hatua zake za kutaka kuhakikisha wadau wake na wananchi kwa ujumla wanakuwa salama kwa kutumia bidhaa zenye ubora, ZBS hufanya ukaguzi wa bidhaa mbalimbali ziingiapo nchini na kuchukua sampuli za bidhaa hizo kwa kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara ili kuhakikisha bidhaa ubora wake kulingana na viwango vilivyowekwa na Taasisi ya Viwango Zanzibar. Kaguzi hizo zinaweza kuwa ni za bidhaa za vyakula, bidhaa za umeme na bidhaa mbalimbali za ujenzi.






ZBS hutumia mifumo miwili mikuu ya ukaguzi (kwa bidhaa zinazoingizwa nchini kutokea nje ya Zanzibar) ambayo ni:

**i) PVoC (Pre-Verification of Conformity)**

PVoC, ni mfumo wa ukaguzi unaofanywa na mawakala wanaofanya kazi ya ukaguzi kwa niaba ya ZBS nje ya nchi inayopima bidhaa kabla hazijaingia nchini. Mawakala hao kwa sasa ni Bureau Veritas na SGS ambao wanapatikana katika nchi mbalimbali Ulimwenguni. Maelezo zaidi kuhusiana na mawakala hao pamoja na ofisi zao duniani kote yanapatikana katika tovuti yetu, www.zbs.go.tz.

**ii) Destination Inspection (DI)**

DI, ni ukaguzi unaofanywa na wakaguzi wa ZBS mara baada ya bidhaa kufika nchini kwa kuchukuliwa sample na kupimwa katika maabara.



### TARATIBU ZA UKAGUZI

Shehena na bidhaa zinazotoka nje ya nchi ambazo hazijakaguliwa kwa ukaguzi wa PVoC kabla ya kusafirishwa na kupewa cheti cha Ubora (CoC), zitakaguliwa na wakaguzi wa ZBS zitapofika nchini kwa mfumo wa DI. Katika ukaguzi huo, ZBS itachukua sampuli ya bidhaa hizo na kuziwasilisha maabara kwa ajili ya uchunguzi na kujiridhisha kuwa zinakidhi matakwa ya viwango vilivyowekwa na Taasisi ya Viwango Zanzibar.

Bidhaa itayobainika kukidhi matakwa ya kiwango husika, muingizaji wa bidhaa hiyo atapatiwa ripoti ya uchunguzi wa maabara pamoja na Cheti cha Ubora wa bidhaa (Batch Certificate) na hatimae kuruhusiwa kuingiza bidhaa hiyo katika soko la Zanzibar kwa ajili ya matumizi yaliyokusudiwa. Orodha ya bidhaa hizo zinazokaguliwa hapa nchini kwa mfumo wa DI inapatikana katika tovuti ya ZBS, www.zbs.go.tz.

Hatua za ukaguzi wa DI ni kama ifuatavyo:-

- Maombi ya ukaguzi
- Ukaguzi wa Shehena na kuchukua sampuli
- Upimaji wa sampuli katika maabara ya ZBS
- Utoaji cheti

# ELIMIKA NA ZBS

## UKAGUZI WA BIDHAA NA MUELEKEO WA UINGIAJI WA BIDHAA BORA

Bidhaa kutoka nje ya nchi ambayo imekaguliwa kwa mfumo wa DI na kuchukuliwa sampuli kwa uchunguzi, haitaruhusiwa kuingia katika soko la Zanzibar, hadi majibu ya uchunguzi wa kimaabara yatakapokuwa yametoka na kuonyesha kuwa bidhaa imekidhi matakwa ya viwango husika. Pindi bidhaa hiyo ikibainika kutokidhi matakwa ya kiwango husika, taratibu stahiki zitachukuliwa kulingana na matokeo ya kiuchunguzi wa kimaabara ikiwemo kupewa barua ya onyo na kutakiwa kufanya marekebisho ya kutorejea kosa hilo au kustahiki adhabu kama itakavyoanishawa hapo chini katika kipengele husika.



Kwa bidhaa ambazo zinakaguliwa nje ya nchi na mawakala wanaofanya kazi kwa niaba ya ZBS, muingizaji wa bidhaa hizo atapaswa kuwasilisha cheti cha (CoC) ambacho hutolewa na mawakala hao wa PVoC kwa bidhaa ambayo itakidhi matakwa ya viwango husika.

Cheti hicho hutumika kuthibitisha ubora wa bidhaa na baada ya kuhakikiwa uhalisia wake (Verification), muingizaji wa bidhaa hiyo, kuruhusiwa kuingiza bidhaa yake katika soko la Zanzibar. Aidha shehena yenye CoC inaweza kuchukuliwa sample na kupimwa/kukaguliwa kwa ajili ya kujiridhisha kuwa taratibu zilifuatwa na mawakala wa PVoC kama inavyotakiwa kwa mujibu wa mkataba husika baina ya ZBS na mawakala hao. Shehena hii itahitaji kutolewa kusambazwa hadi ripoti ya ukaguzi na upimaji wa kimaabara itakapotolewa na kubainika kuwa imekidhi matakwa ya kiwango husika.

### TARATIBU ZA UKAGUZI WA VYOMBO VYA MOTO

Katika ukaguzi wa vyombo vya moto, ZBS imeipa kipaumbele ukaguzi huu ili nchi yetu isigeuzwe jalala la vyombo hivyo vilivyotumika visivyofaa kwa matumizi ya barabarani. ZBS ilianzisha utaratibu wa kukagua na kupima magari hayo kabla hayajasafirishwa kuja nchini. Awali Waagizaji wote walitakiwa kukagua na kupima magari yao kabla ya kuyasafirisha kuja nchini. Kwa sasa Taasisi ya Viwango Zanzibar imejipanga na kufanya ukaguzi huo hapa hapa nchini na kuwa na uweledi wa kukagua na kujiridhisha kwa kutoa cheti cha kuthibitisha ubora wa bidhaa hii.



### ADHABU ZA KUTOZINGATIA PVoC

Taratibu za upimaji wa PVoC ulianza rasmi mwaka 2016 ambapo njia mbalimbali zilitumika katika kuhamasisha kutumia njia hii ya PVoC taratibu zilielezwa kuwa shehena zote zisizo na CoC zinatozwa faini ya PVoC. Kwa utaratibu wa ukaguzi wa bidhaa zinapoingia yaani Destination Inspection (DI). Shehena zisizokidhi matakwa ya viwango zitarejeshwa katika nchi zinakotoka au kuharibiwa kwa gharama ya mwingizaji. Ili kuepuka kadhia hii, waagizaji wote wa bidhaa wanapaswa kuhakikisha kuwa shehena zao zinathibitishwa na mawakala wa ukaguzi wa ZBS ambao wana ofisi kote duniani.

# ELIMIKA NA ZBS

## UKAGUZI WA BIDHAA NA MUELEKEO WA UINGIAJI WA BIDHAA BORA

Muingizaji wa mzigo atalazimika kurudisha bidhaa itakayogundulika kutokidhi matakwa ya viwango katika nchi alikotoa bidhaa hiyo au kulipia gharama za uteketezaji wa bidhaa husika kama uteketezaji wake hauna athari kwa mazingira.





ZBS ilianza kutekeleza udhibiti wa ubora wa bidhaa zinazoingizwa nchini kutoka nje kwa nia ya kulinda nchi yetu isiwe jalala la bidhaa duni. Katika Kuhakikisha kuwa bidhaa zote zinakidhi matakwa ya viwango husika kabla ya kusafirishwa kuja nchini mambo yakuzingitia ni kama yafuatayo:-

- Bidhaa zinazoagizwa na kusafirishwa kuja Zanzibar zilizopo kwenye orodha ya bidhaa zinazotakiwa kukaguliwa kabla ya kusafirishwa kuja nchini ni lazima zikaguliwe na kupewa cheti cha ubora (CoC) kama uthibitisho wa kukidhi Viwango.
- Cheti cha uthibiti wa kukidhi Viwango ni lazima ili kuruhusiwa kuchukua mzigo wako Bandarini au Uwanja wa Ndege.
- Bidhaa ambazo hazipaswi kukaguliwa kabla ya kusafirishwa zitakaguliwa na maafisa wa Taasisi ya Viwango Zanzibar baada ya kufika nchini.
- Msafirishaji atabeba dhamana ya mzigo wowote utakaoingizwa nchini bila cheti cha ubora (CoC).
- Ni jukumu la mwagizaji, msambazaji/muuzaji au mzalishaji wa bidhaa kuhakikisha bidhaa zake zinakidhi Viwango.

Ili mteja au muingizaji akitaka kuingiza mzigo wake nchini na ili apate cheti cha ubora wa bidhaa yake ni lazima azingatie kuwa:-

- Achague wakala wetu ambaye anataka akague shehena yake. Anuani za mawakala wetu zinapatikana kwenye tovuti yetu www.zbs.go.tz.
- Awasilishe fomu ya kuomba ukaguzi iliyokwishajazwa ikiambatanishwa na Ankara kifani (preforms invoice).
- Awasilishe ripoti ya maabara vyeti vya umahiri vya maabara.

### MALIPO STAHIKI YA UKAGUZI

| NA | MAELEZO | KIASI |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya maombi | **TZS**. 10,000 |
| 2. | Ada ya Ukaguzi | **TZS**. 50,000 |
| 3. | Ada ya Upimaji | Hutofautiana kulingana na bidhaa husika |
| 4. | Ada ya udhibiti wa shehena | Asilimia 2% FoB ya thamani ya mzigo na gharama za usafirishaji |